# UCHAMBUZI
# WA
# KITABU
# CHA
# **“WARAKA KWA WAEBRANIA”**

**Na Ap Shemeji Melayeki**

## **Siku ya 1**
## **UTANGULIZI**

Karibuni katika semina ya Neno la Mungu tukiangazia kwa umakini kitabu cha Waebrania.

Semina hii itakuwa ikifanyika kwa njia ya *Whatsapp Groups* kila siku saa Moja jioni hadi saa 3 usiku, na kufuatiwa na Facebook Live Session kwenye Page ya **Apostle Shemeji Melayeki*** **saa** 3 kamili usiku hadi saa 4 usiku.

Kila siku ya Ijumaa na Jumapili hatutafanya Facebook live wala Whatsapp ila tutakutana Singo Garden mkabala na Mbezi garden Hotel kwa ajili ya kujifunza na kuomba pamoja kwa wale walioko Dar es Salaam na wengine watakuta audio za mafundisho Youtube.
Ijumaa ni saa 12 jioni na Jumapili ni saa 5 asubuhi…. Singo Garden mkabala na Mbezi garden Hotel..

Sessions zote za Facebook Live pia zitawekwa Youtube ya **Apostle Shemeji Melayeki**

KARIBUNI TUJIFUNZE….

***MAMBO YA MSINGI***

Kila kitabu kwenye Biblia hakitafsiriwi chenyewe bali kwa kupitia vitabu vingine hii ni kwa sababu Biblia toka Mwanzo mpaka Ufunuo ni kitabu kisichojipinga hasa kikitumiwa na kutafsiriwa ipasavyo.

Kitabu hiki kama Nyaraka zingine zinachukua msingi wa maelezo yake kwenye maandiko (yaani vitabu vya Agano la Kale) hivyo ni tafsiri ya mambo ambayo Mungu alisema kwa vinywa vya manabii wake zamani kwa habari ya Ufunuo wa Kristo. (nitaelezea huko mbele)…

Njia nzuri ya kutafsiri maandiko ni kwa kutumia maandiko, (andiko hutafsiri andiko) siyo kutumia mawazo ya mtu yeyote au falsafa yoyote. BIBLIA INAJITOSHELEZA…

Ni vyema ukatenga muda wa kufuatilia sessions hizi kwa umakini bila kuruka session yoyote ikiwa unataka kupata mtiririko sahihi wa uchambuzi wa mwalimu. Usianze sehemu ya 10 kabla hujasikiliza, kusoma au kutazama ya 9… yaani fuata mfululizo. Ukirukia katikati au mwisho unaweza usielewe kinachoendelea.

***JUU YA KITABU CHA “WARAKA KWA WAEBRANIA”***

Mambo kadhaa ya kutazama kabla ya kwenda kwenye kitabu hiki…
Kitabu kama ilivyo jina lake Imeandikwa kwa Waamini Waebrania.

Mtindo wa uandishi wa kitabu hiki unaonyesha kuwa hakuna sura inayojitegemea bali Mwandishi amepanga maelezo yake hatua kwa hatua.. ndiyo maana ni shida sana kwa watu wengi kuelewa kitabu hiki kwani huishia kuchanganyikiwa au kuvuruga lengo lake kwa kuanzia sura ya 11, 12 au 13 ambazo mara nyingi hutumika kufundishia. ANGALIA JINSI KILA SURA INAVYOANZA. HII INAONYESHA KUWA KILA SURA INATEGEMEA MAELEZO YA SURA YA (ZA) NYUMA.
Waebrania 1:1 [1]Mungu,
Waebrania 2:1 [1]Kwa hiyo
Waebrania 3:1 [1]Kwa hiyo,
Waebrania 4:1 [1]Basi,
Waebrania 5:1 [1]Maana kila kuhani mkuu
Waebrania 6:1 [1]Kwa sababu hiyo,
Waebrania 7:1 [1]Kwa maana Melkizedeki huyo,
Waebrania 8:1 [1]Basi, katika hayo tunayosema,
Waebrania 9:1 [1]Basi hata agano la kwanza
Waebrania 10:1 [1]Basi torati,
Waebrania 11:1 [1]Basi imani
Waebrania 12:1 [1]Basi na sisi pia,
Waebrania 13:2 [2]Msisahau

Kitabu hiki kimejikita kufundisha habari za Mungu kwa Ufunuo wa Yesu Kristo. Kwa mtiririko unaoeleweka mwandishi ametumia zaidi maneno ya kufananisha (COMPARISON) Yesu na watu au vitu vilivyotumiwa kwenye maandiko (Mwanzo hadi Malaki) akimfananisha Yesu na vitu au watu hao kwa lengo la kuonyesha UKUU AU UBORA ULIOKO NDANI YA YESU KRISTO.. maneno ***BORA**** YAMETUMIKA ZAIDI…

*BORA.... ZA KITABU CHA WAEBRANIA...*

Waebrania 1:4
(YESU) [4]amefanyika *bora kupita malaika,* kwa kadiri jina aliloliríthi lilivyo _tukufu kuliko lao._

Waebrania 7:22
[22]basi kwa kadiri hii Yesu amekuwa *mdhamini wa agano lililo bora zaidi.*

Waebrania 8:6-7
[6]Lakini sasa amepata *huduma iliyo bora zaidi,* kwa kadiri alivyo *mjumbe wa agano lililo bora,* lililoamriwa juu ya *ahadi zilizo bora.*
[7]Maana kama _lile la kwanza lingalikuwa halina upungufu, nafasi isingalitafutwa kwa lile la pili._

Waebrania 9:23
[23]Basi ilikuwa sharti nakala za mambo yaliyo mbinguni zisafishwe kwa hizo, lakini mambo ya mbinguni yenyewe yasafishwe kwa *dhabihu zilizo bora kuliko hizo.*

Waebrania 11:4
[4]Kwa imani Habili alimtolea Mungu *dhabihu iliyo bora kuliko Kaini;* kwa hiyo alishuhudiwa kuwa ana haki; Mungu akazishuhudia sadaka zake, na kwa hiyo, ijapokuwa amekufa, _angali akinena._

Waebrania 11:16
[16]Lakini sasa waitamani *nchi iliyo bora,* yaani, ya mbinguni. Kwa hiyo Mungu haoni haya kuitwa Mungu wao; maana *amewatengenezea mji.*

Waebrania 11:35
[35]Wanawake walipokea wafu wao waliofufuliwa. Lakini wengine waliumizwa vibaya hata kuuawa, _wasikubali ukombozi,_ ili wapate *ufufuo ulio bora;*

Waebrania 11:40

[40]kwa kuwa Mungu alikuwa _ametangulia kutuwekea sisi_ *kitu kilicho bora,* ili wao _wasikamilishwe pasipo sisi._

NI VYEMA TUKAONA YA KWAMBA MWANDISHI ALIMFANANISHA

1. YESU NA MALAIKA
2. YESU NA MUSA
3. YESU NA YOSHUA
4. YESU NA MELKIZEDEKI
5. YESU NA MAKUHANI
6. YESU NA WAZEE WA ISRAELI
7. YESU NA SADAKA (MAMBO YA IBADA) ZA WAYAHUDI

*(MAMBO HAYA TUTAYACHAMBUA KWA UNDANI ZAIDI HUKO MBELE)*
Kujifunza vitu hivi kwa umakini utatusaidia kuuona wokovu wa Mungu kwa wanadamu kama ambavyo Yesu aliwaambia wanafunzi wake kuwa Musa, manabii na Zaburi waliandika habari zake.. Kusoma Musa anamaanisha vitabu vitano vya kwanza kwenye Biblia (Mwanzo, Kutoka, Mambo ya Walawi, Hesabu na Kumbukumbu la Torati)… Vitabu hivi hujenga msingi wa wokovu wa wanadamu kama ikitazamwa sawa sawa na kwa umakini wake.

**ANGALIA…** Yesu alipowatokea Kleopa na mwenzake wakati wanaelekea Emau aliwaambia..
Luka 24:25-27
[25]Akawaambia, Enyi msiofahamu, wenye mioyo mizito ya kuamini ***yote waliyoyasema manabii!***
[26]Je! Haikumpasa Kristo kupata mateso haya na kuingia katika utukufu wake?
[27]Akaanza kutoka Musa na manabii wote, akawaeleza katika maandiko yote mambo yaliyomhusu yeye mwenyewe.

ANGALIA MSISITIZO WA NENO YOTE… *IMEMPASA Kristo kupata mateso YALE na kuingia katika utukufu wake* Huu ni ujumbe mkuu au summary ya ujumbe wa *MUSA NA MANABII WOTE….*

[27]Akaanza kutoka Musa na manabii wote, akawaeleza katika maandiko yote mambo yaliyomhusu yeye mwenyewe.
Angalia msisitizo * MUSA NA **MANABII _*WOTE*_*** waliandika habari zinazomhusu KRISTO… Huu mstari wa 27 haina maana Yesu alisema hivyo ila ni JUMLA YA ALICHOWAELEZA… ina maana Yesu alipita vitabu vya Musa na Manabii akiwaonyesha HATUA KWA HATUA MAMBO YALIYOMHUSU kwa HABARI YA **KUTESWA, NA KUINGIA KATIKA UTUKUFU WAKE**

Kisha baadaye akakutana na wanafunzi wake akawaambia…

Luka 24:44-47
[44]Kisha akawaambia, Hayo ndiyo maneno yangu niliyowaambia nilipokuwa nikali pamoja nanyi, ya kwamba ni lazima yatimizwe yote niliyoandikiwa katika Torati ya Musa, na katika Manabii na Zaburi.
[45]Ndipo akawafunulia akili zao wapate kuelewa na maandiko.
[46]Akawaambia, Ndivyo ilivyoandikwa, kwamba Kristo atateswa na kufufuka siku ya tatu;
[47]na kwamba mataifa yote watahubiriwa kwa jina lake habari ya toba na ondoleo la dhambi, kuanza tangu Yerusalemu.

Hii ina maana kuwa mambo ambayo Yesu aliyasema kwenye vitabu vya Injili (Mathayo, Marko, Luka na Yohana) kabla ya kuteswa na kufufuka yalikuwa YANAHUSU KUTESWA NA KUFUFUKA KWAKE SIKU YA TATU… na hayo yapo kwenye *Torati ya Musa, na katika Manabii na Zaburi.*

Hapo sasa macho yao yakafunguliwa, NI KAMA AHAAA…. KUMBE… DAAH HATA HATUKUELEWA…

Mstari wa 47 unaonyesha lengo la KUFA NA KUFUFUKA KWAKE…. WATU WAHUBIRIWE HABARI YA TOBA NA ONDOLEO LA DHAMBI…

Ni muhimu kujua kuwa FOCUS au mkazo wa maandiko ni kumfunua Yesu Kristo kwa nguvu sana. Yesu anaonyesha kuwa Musa (aliyeandika vitabu vitano vya mwanzo katika Biblia), manabii na Zaburi, wote waliandika juu ya MATESO YA YESU KRISTO, KUFA NA KUTUKUZWA KWAKE NA KWAMBA ONDOLEO LA DHAMBI LITAHUBIRIWA KWA SABABU HIYO..

PETRO NAYE ALIKAZIA UJUMBE HUO HUO…
Matendo ya Mitume 3:22-24
[22]Kwa maana ***Musa*** kweli alisema ya kwamba, Bwana Mungu wenu atawainulieni nabii, katika ndugu zenu, kama mimi; msikieni yeye katika mambo yote atakayonena nanyi.
[23]Na itakuwa ya kwamba kila mtu asiyemsikiliza nabii huyo ataangamizwa na kutengwa na watu wake.
[24]Naam, na ***manabii wote tangu Samweli na wale waliokuja baada yake, wote walionena, walihubiri habari za siku hizi.***

Angali hapo, TANGU *SAMWELI* WALINENA!.... HABARI ZA SIKU HIZO NI ZIPI? *MATESO YA YESU KRISTO, KUFA NA KUTUKUZWA KWAKE NA KWAMBA ONDOLEO LA DHAMBI LITAHUBIRIWA KWA SABABU HIYO..*

Huu ndio ujumbe mkuu wa vitabu vya Agano la Kale (Maandiko Matakatifu) kama Yesu na mitume walivyotafsiri..

SASA TUANGALIE…